
# Kifua Kikuu: pata ukweli!

## Kifua Kikuu ni nini?

Kifua Kikuu (TB) ni ugonjwa ambao kwa kawaida huathiri mapafu. Kifua Kikuu wakati mwingine huathiri sehemu nyengine za mwili, kama vile ubongo, figo, au uti wa mgongo. Ugonjwa wa Kifua Kikuu unaweza kusababisha kifo usipotibiwa.

## Kifua Kikuu husambazwa vipi?

Viini vya Kifua Kikuu husambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kupitia hewa. Viini vya Kifua Kikuu huwekwa hewani wakati mtu aliye na ugonjwa wa Kifua Kikuu anakohoa, kupiga chafya, kucheka, au kuimba. Kifua Kikuu HAKISAMBAZWI kwa kushiriki vyombo au vikombe, au kubadilishana mate wakati wa kumbusu mtu.



## Dalili za Kifua Kikuu ni zipi?

Watu walio na ugonjwa wa Kifua Kikuu mara nyingi hujisikia wakiwa wanyonge au wagonjwa, hupoteza uzito, wana joto mwilini, na hutokwa na jasho usiku. Ikiwa ugonjwa wao wa Kifua Kikuu uko mapafuni, wanaweza pia kukohoa na kuumwa na kifua, na wanaweza pia kukohoa damu. Dalili zingine hutegemea sehemu ya mwili iliyoathirika.

ASET 5/09

## Tofauti kati ya ugonjwa wa Kifua Kikuu na uambukizo wa Kifua Kikuu ni nini?

Watu walio na **ugonjwa** wa Kifua Kikuu ni wagonjwa kutokana na idadi kubwa ya viini vya vya Kifua Kikuu vilivyohai katika miili yao. Kwa kawaida huwa wana moja au zaidi ya dalili za ugonjwa wa Kifua Kikuu. Watu hawa wanaweza kusambaza viini vya Kifua Kikuu kwa wengine. Ugonjwa wa Kifua Kikuu unaweza pia kusababisha madhara ya kudumu mwilini na kifo. Watu hawa hupewa dawa zinazoweza kutibu Kifua Kikuu.

Watu walio na uambukizo wa Kifua Kikuu pia wana viini vinavyosababisha Kifua Kikuu mwilini mwao. Lakini wao **sio wagonjwa** kwa sababu viini sio vingi sana, na viini vimejituliza mwilini mwao. Hawawezi kusambaza viini kwa wengine. Hata hivyo, watu hawa wanaweza kupata ugonjwa wa Kifua Kikuu baadaye, haswa wakiwa katika mojawapo ya vikundi vilivyo hatarini sana vilivyoorodheshwa kwenye sehemu ya “Nani hupata ugonjwa wa Kifua Kikuu?” Watu walio na viini vya Kifua Kikuu wanaweza kutumia madawa kuwazuia wasipate ugonjwa wa Kifua Kikuu.

## Nani hupata ugonjwa wa Kifua Kikuu?

Mtu anapopata uambukizo wa Kifua Kikuu, yeye huwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kupata ugonjwa wa Kifua Kikuu ikiwa mtu huyo

- Ameambukizwa Virusi vya UKIMWI
- Ameambukizwa viini vya Kifua Kikuu hivi majuzi (katika miaka miwili iliyopita)
- Ana matatizo mengine ya afya, kama vile kisukari, yanayofanya iwe vigumu kwa mwili kupigana na viini
- Anatumia pombe au kujidunga madawa haramu
- Hakutibiwa ipasavyo kwa uambukizo wa Kifua Kikuu hapo mbeleni

## Ninawezaje kujua ikiwa nina Kifua Kikuu?

Pata kipimo cha ngozi cha Kifua Kikuu au kipimo cha damu cha QuantiFERON®-TB Gold (QFT). Ikiwa mojawapo ya vipimo itaonyesha uwepo, yawezekana sana kuwa utapewa vipimo vingine kuthibitisha ikiwa una uambukizo wa Kifua Kikuu au ugonjwa wa Kifua Kikuu.

## Ninaweza kupata wapi kipimo cha ngozi cha Kifua Kikuu au QFT?

Unaweza kupata kipimo cha ngozi cha Kifua Kikuu kutoka kwa daktari wako au kituo cha afya kilicho karibu nawe. Yawezekana ukapata kipimo cha QFT kwenye kituo cha afya kilicho karibu nawe.

## Vipimo vya Kifua Kikuu hufanywa vipi?

Kwa kipimo cha ngozi cha Kifua Kikuu, mhudumu wa afya hutumia sindano ndogo kuweka kiini cha kupima, kiitwacho ‘tuberculin’, chini ya ngozi yako. Hii kwa kawaida hufanywa kwenye sehemu ya chini na ndani ya mkono wako. Baada ya kupata kipimo, lazima urudi baada ya siku mbili hadi tatu kuangaliwa ikiwa kuna athari kwa kipimo. Ikiwa kuna athari, ukubwa wa athari utapimwa.



Ikiwa kituo chako cha afya kinatoa kipimo cha QFT, damu yako kidogo huchukuliwa kufanya kipimo. Utaelezewa jinsi ya kupata matokeo ya kipimo chako.


## Na je, kipimo kisipoonyesha uwepo?

Kipimo cha ngozi kisichoonyesha uwepo kwa kawaida humaanisha kuwa hujaambukizwa. Hata hivyo, kipimo kinaweza kutoonyesha uwepo kimakosa ikiwa umeambukizwa hivi majuzi. Inachukua wiki mbili hadi kumi baada ya kuambukizwa kwa kipimo chako cha ngozi kuonyesha uwepo. Kipimo pia chaweza kutoonyesha uwepo kimakosa ikiwa kinga yako ya mwili haifanyi kazi barabara.

Kipimo cha QFT kisichoonyesha uwepo, kwa kawaida humaanisha kuwa hujaambukizwa.

## Na je, kipimo kikionyesha uwepo?

Kipimo cha ngozi au cha QFT kuonyesha uwepo kwa kawaida humaanisha kuwa umeambukizwa viini vya Kifua Kikuu. Haimaanishi kuwa sharti una ugonjwa wa Kifua Kikuu. Vipimo vingine, kama vile picha ya kifua au sampuli ya makohozi, huhitajika kuchunguza ikiwa una ugonjwa wa Kifua Kikuu.



## Na ikiwa nilipata chanjo ya BCG?

BCG ni chanjo dhidi ya Kifua Kikuu. Chanjo hii haitumiki sana Marekani, lakini mara nyingi hupatiwa kwa watoto wadogo katika nchi nyingine ambako Kifua Kikuu huonekana kwa wingi. Chanjo ya BCG kwa kawaida haiwalindi watu wazima dhidi ya Kifua Kikuu. Unaweza bado kupata uambukizo au ugonjwa wa Kifua Kikuu. Hata kama ulipata chanjo ya BCG, utahitaji kipimo cha ngozi cha Kifua Kikuu au QFT kuchunguza ikiwa unaweza kuwa na uambukizo au ugonjwa wa Kifua Kikuu.

ASET 5/09

## Nifanye nini ikiwa nina uambukizo au ugonjwa wa Kifua Kikuu?

Pata vipimo vinavyohitajika vya kufuatilia. Fuata ushauri wa daktari wako na utumie madawa kama ilivyoagizwa. Hivi leo, maambukizo ya Kifua Kikuu na ugonjwa wa Kifua Kikuu unaweza kutibiwa na kuponyeka kwa dawa.




Kwa maelezo zaidi kuhusu Kifua Kikuu au kupata kipimo cha ngozi cha Kifua Kikuu, mpigie simu daktari wako au kituo cha afya kilicho karibu nawe.

Kwa habari zaidi kuhusu Kifua Kikuu tembelea:

Tovuti ya Kitengo cha CDC
Kuondoa Kifua Kikuu iliyo
www.cdc.gov/tb

# Kifua Kikuu



# pata ukweli

IDARA YA AFYA NA HUDUMA ZA KIBINADAMU
Kituo cha Kudhibiti na
Kuzuia Magonjwa (CDC)

TBgtfcts_Swahili.indd 2 5/14/2009 5:08:40 PM